JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Simu/Fax : +255 232935205
Barua pepe : **dakawatc@gmail.com**

Chuo Cha Ualimu Dakawa
S. L. P. 944
MOROGORO.

Kumb. Na. ***DKWTC/JSTR/VOL.1/***

Tarehe 29/04/2021

Ndugu……..…….
S.L.P. ……..……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA ASTASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI (ENGLISH MEDIUM) NA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU SEKONDARI KWA MWAKA 2021/2022.

1.0 UTANGULIZI

Napenda kukupongeza na kukuarifu kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuchagua kujiunga na Mafunzo ya Ualimu ngazi ya

i. Astashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi (English Medium) kuanzia tarehe **15 Julai, 2021**.
ii. Stashahada ya Ualimu Elimu ya Sekondari kuanzia tarehe **15 Agosti, 2021**.

Ukiwa Chuoni utapatiwa muda wa kufanya Mazoezi ya kufundisha kulingana na kalenda ya chuo na maelekezo ya Wizara.

1.1 MAHALI CHUO KILIPO

Chuo hiki kipo **Mkoa wa Morogoro,** Wilaya ya Kilosa, Umbali wa kilometa **60** kutoka Morogoro Mjini, Barabara Kuu iendayo **Dodoma.**

1.2 NAMNA YA KUFIKA CHUONI

Ukifika Morogoro Stendi ya basi **MSAMVU,** uliza stendi ya magari madogo (Daladala au Noah) yaendayo **DUMILA** Shuka njia panda ya **VETA,** chukua usafiri wa pikipiki, wakulete chuo cha Ualimu Dakawa, umbali wa kilometa nne (**4)** tu toka barabara kuu. Nauli ya pikipiki si zaidi ya **Tshs. 2,000/=** AU

Ukitokea Dodoma; Shuka njia panda ya **VETA**, kisha chukua pikipiki ikulete chuo cha Ualimu Dakawa, umbali wa kilometa nne (**4)** tu toka barabara kuu. Nauli ya pikipiki si zaidi ya **Tshs. 2,000/=**

Unashauriwa kufika mapema kabla ya saa 11:00 jioni kwa ajili ya usalama wako.

2.0 MAFUNZO

Kwa wanachuo wa Astashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi (English Medium), chuo kitafunguliwa tarehe **15/07/2021** na mwisho wakufika chuoni ni tarehe **30/07/2021**. Wanachuo wa Stashahada ya Ualimu Elimu Sekondari, chuo kitafunguliwa tarehe **15/08/2021** na mwisho wakufika chuoni ni tarehe **30/08/2021.** Ukiwa hapa chuoni katika kila Muhula utatakiwa kufanya Mazoezi, majaribio, na

Mitihani ya ndani na kufaulu. Utakapofika chuoni nenda **Ofisi ya Usajili** ambapo utapata maelekezo na taratibu zote za chuo na kusajiliwa.

3.0 MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI

3.1 Vyeti na Vitambulisho

Unatakiwa kuja na nyaraka zifuatazo ili usajiliwe

a) Barua ya kuitwa kujiunga na mafunzo ya Ualimu (Joining Instruction)
b) **Vyeti HALISI** (Academic na Leaving Certificates) vya Kidato cha **nne** na Kidato cha **sita.**
c) Cheti cha kuzaliwa (Original birth certificate)
d) Walioajiriwa walete barua kutoka kwa Waajiri wao ya kuruhusiwa kuhudhuria mafunzo.
e) Uje pia na vivuli **(photocopies)** vya vyeti vyako vyote.
f) Hakikisha umepimwa na Daktari wa Hospitali ya Serikali na kujaziwa fomu iliyoambatanishwa kwenye barua hii ya kuthibitisha hali ya Afya yako.
g) Pia kumbuka kuja na passpoti size mbili.

3.2 ADA

Ada ya mwaka ni **TShs. 450,000/=** au **225,000/=** kwa muhula. Ada hiyo italipwa kwa kutumia mfumo wa **Control number** ambayo utapewa ufikapo chuoni.

3.3 MICHANGO

Hakikisha unalipa michango yote ifuatayo kwenye **Akaunti Namba 01J1048471300; DAKAWA T.C - SELF RELIANCE A/C - CRDB. Mandela Branch Morogoro (*Pia unaweza kulipia katika Tawi lolote la CRDB nchini*)**

S/N	MCHANGO	KIASI	MAONI
1	Serikali ya wanachuo	5,000/=	Kwa Mwaka
2	Huduma ya kwanza	10,000/=	Kwa Mwaka
3	Usafi na mazingira	20,000/=	Kwa Mwaka
4	Kukodisha godoro	10,000/=	Kwa Mwaka
5	Usajili na Kitambulisho	20,000/=	Kwa Mwaka wa kwanza tu
6	Michezo	30,000/=	Kwa Mwaka
7	Ulinzi	30,000/=	Kwa Mwaka
8	Ukarabati	25,000/=	Kwa Mwaka
	JUMLA	**150,000/=**	

NB:-

i) Hakikisha umelipa michango yote kama ilivyooneshwa hapo juu. Na kuja na Bank Pay- in Slip chuoni.

ii) Uje na kitambulisho cha Bima ya afya na fedha ya kujikimu.

iii) Fedha Taslimu Haitapokelewa na fedha ikishalipwa **HAIRUDISHWI.**

iv) Wakati wa likizo baadhi ya wanachuo hubakizwa kwa ajli ya Elimu ya Kujitegemea na kutunza mazingira ya chuo.

3.4 SARE YA CHUO

WANAUME

a) Suruali mbili za rangi nyeusi zenye mashono ya heshima, mifuko mitatu, rinda mbili na turn up.
b) Mashati mawili ya mikono mirefu rangi ya blue bahari (**Light blue)**. Uje na fedha Tshs **15,000/=** kwa ajili ya T-shirt moja (1) yenye nembo ya chuo.
c) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika, vitavaliwa na soksi wakati wote.
d) Tai ndefu nyeusi na koti jeusi (suti)

WANAWAKE

a) Sketi mbili nyeusi- ndefu zenye mshono wa mapande sita (6) (kitambaa cha suti) zisizo na mpasuo, zinazovuka magoti nchi tatu.
b) Mashati mawili ya mikono mirefu rangi ya bluu bahari (**Light blue)**. Uje na fedha Tshs **15,000/=** kwa ajili ya T-shirt moja (1) yenye nembo ya chuo.
c) Tai fupi nyeusi (sio butterfly tie) na koti jeusi (Suti).
d) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika vyenye visigino vifupi vitakavyovaliwa na soksi nyeupe.
e) Watakaopenda kuvaa Hijab watumie rangi ya Light Blue (*Ifanane na shati*).

4.0 MAVAZI MUHIMU KWA WOTE.

a) Tracksuit ya bluu, T-shirt ya bluu, raba pamoja na nguo nyingine za michezo kama bukta, fulana, sketi n.k
b) Mavazi mengine yote utakayokuja nayo, nje ya sare yawe ya mashono ya ***Heshima*** *na* ***yanayoakisi Taaluma ya Ualimu***. (Mavazi hayo yatakaguliwa ofisi ya Usajili)

5.0 MAHITAJI MUHIMU

5.1 MALAZI.

a) Blanketi, shuka mbili za light blue na foronya za light blue, mto pamoja na chandarua kwa ajili ya kujikinga na mbu.
b) Vyombo vya chakula –sahani, bakuli, kikombe **(visiwe vya plastic),** kijiko, galoni ya plastiki ya lita 5 ya kuhifadhia maji yako ya kunywa.
c) Ndoo ya kuogea. (*Hupatikana pia katika maduka yaliyopo karibu na chuo)*
d) Tochi yenye betri kwa ajili ya tahadhari ya kukosekana kwa umeme.
e) Pazia light blue urefu wa ft. 9 kwa ft. 3.5 kwa ajili ya chumba chako.

5.2 TAALUMA

a) Daftari kubwa zisizopungua 10 kwa muhula (kaunti book Quare 2) *(hupatikana pia katika maduka yaliyopo karibu na chuo.*
b) Vitabu mbalimbali na Mihtasari ya michepuo ya masomo yako uliyochaguliwa

c) Rimu moja ya karatasi nyeupe aina ya NO 1/mondi nyeupe (A4 photocopy paper) kwa ajili ya shughuli za kitaaluma. Hii hutolewa kila mwaka *(Hupatikana pia katika maduka yaliyopo karibu na chuo).*

d)

Kwa mwanachuo unayechukua somo la Hisabati uje na scientific calculator na mathematical table.

NB: Kumbuka kufika na sanduku imara lenye kufuli kwa utunzaji salama wa vifaa vyako vyote, pia kumbuka kuja na rimu moja kwa ajili ya matumizi yako binafsi

6. MWISHO:

Baada ya kusoma maagizo haya, jaza fomu iliyoambatanishwa na kukamilisha. Ufikapo chuoni utakabidhiwa nakala ya sheria, kanuni za taratibu za Chuo.Pia utatakiwa kukiri au kukubali nafasi hiyo ya mafunzo kwa kujaza fomu.

"Ualimu bora huanzia chuoni; Tunakutegemea kuwa Mwalimu bora tangu mwanzo wa mafunzo yako".

KARIBU SANA CHUO CHA UALIMU DAKAWA

NAILEJILEJI S. JACOB
MAKAMU MKUU WA CHUO
0756 484454

Nakala: Mkurugenzi Elimu ya Ualimu,
Wizara ya Elimu Sayansi, Teknolojia,
S .L .P .10
40479 DODOMA

Makamu Wa Chuo
Chuo Cha Ualimu Dakawa
MOROGORO

GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A

To:
The Medical Officer
……..
……...
……..

Mr/Mrs/Miss ……
(Name in full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teacher training course.
The examination should include the following categories (i – ii) each category or sub category of which will render the applicant ineligible in case of a defect.

Primary/category iv will also render a girl candidate ineligible for the course:-

i. (a) Eye-sight (b) Hearing (c) Limbs (d) Speech
   (e) Venereal disease (f) Leprosy (g) Epilepsy
ii. Neuroses
iii. Other serious diseases
iv. Pregnancy

MEDICAL CERTIFICATE

PART B: (To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that he/she is physical fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time teacher training course.

i. (a) Eye-sight…… (b) Hearing…… (c) Limbs ……
   (d) Speech……. (e) Venereal diseases…….
   (f) Leprosy …… (g) Epilepsy……
ii. Neuroses ……
iii. Serious diseases……..
iv. Pregnancy

Date …….. **Signature** ……

Station …… **Designation** …….